Ohio | Department of Medicaid

Tarehe 22 Machi, 2019

**Kwa Mtumiaji wa mpango wa Medicaid,**

Wahudumu wa Medicaid katika Jimbo la Ohio wataboresha zaidi (angalia jedwali) mpango unaojulikana kama Electronic Visit Verification (EVV). Rekodi zetu zinaonesha kwamba wewe hupokea baadhi ya huduma hizi. EVV itanakili wakati huduma hizi zitaanza rasmi na kukamilika. Hatua hii inasaidia Medicaid kulipia huduma unazopokea. Unatajumuishwa kwenye mpango huu ikiwa unapokea huduma za EVV ambazo zimelipiwa na walipaji wafuatao: Idara ya Medicaid ya Ohio (ODM), Idara ya Ulemavu ya Jimbo la Ohio (DODD), Idara ya Uzee (ODA) au Mipango ya Managed Care.

Huenda una kifaa kidogo nyumbani mwako ambacho mtoaji huduma atajaza anapowasili au anapoondoka. Kifaa chenyewe kinafanana na simu mahiri, lakini kamera zake zimezimwa kabisa. Maikrofoni hutumika tu wakati kifaa hiki kinanasa sauti ya kuthibitisha utoaji wa huduma.

Watoaji huduma wataweza kutumia kifaa cha EVV popote ulipo. Wahudumu wako watatia saini wanapowasili na wanapoondoka baada ya kukupa hudumu unazohitaji. Unaweza kubeba kifaa chako cha EVV ikiwa utapokea huduma mbali na nyumba yako.

Kifaa cha EVV kinapatikana bila malipo kwako na kwa wahudumu wako. Wahudumu wanaweza kuanza mafunzo tarehe 6, Mei 2019 na wataweza kuanza kutumia EVV baada ya mafunzo kukamilika. Mtoaji huduma wako anawajibika kwa kutumia EVV. Mhudumu wako ataagiza kifaa hiki na utakipokea kwenye barua pepe. Wakati mhudumu wako hatakihitaji kifaa hiki kwa EVV, utapokea kikasha cha kurudisha kifaa hiki kwenye barua pepe bila malipo. Mchakato huu unakusudiwa kuwa rahisi.

Kwa maelezo zaidi, tafadhali tembelea http://medicaid.ohio.gov/EVV usome Maswali Yanayoulizwa Mara Nyingi na utazame video kuhusu EVV.  Unaweza pia kupata nyenzo zaidi kuhusiana na EVV hapa.

Ikiwa una swali lolote, tafadhali wasiliana na watoaji huduma wako au msimamizi wa huduma yako, ikiwa unaye. Unaweza pia kupiga simu kwa nambari 1-800-324-8680 ya Usaidizi wa Dharura kwa Watumiaji wa Medicaid.

Mwaminifu,

Idara ya Medicaid ya Jimbo la Ohio

50 W. Town Street, Suite 400
Columbus, Ohio 43215
medicaid.ohio.gov

An Equal Opportunity Employer and Service Provider

<table>
<tr><td rowspan="2">AWAMU YA 1<br><br>HUDUMA</td><td>Ilitekelezwa tarehe 8 Januari, 2018</td></tr>
<tr><td>Mpango wa EVV kwa huduma zinazogharamiwa moja kwa moja na Medicaid katika huduma isiyolipishwa:<br><br>▪ Msaidizi wa Afya wa Nyumbani wa Mpango wa Jimbo<br>▪ Uuguzi wa Afya wa Nyumbani wa Mpango wa Jimbo<br>▪ Tathmini ya RN ya Mpango wa Jimbo<br>▪ Uuguzi wa Ondoleo la Huduma ya Nyumbani ya Ohio (OHCW)<br>▪ Msaidizi wa Huduma ya Kibinafsi wa OHCW<br>▪ Mhudumu wa Huduma ya Nyumbani wa OHCW<br>▪ Tathmini ya RN wa OHCW<br>▪ Uuguzi wa Zamu ya Faragha (PDN)</td></tr>
</table>

<table>
<tr><td rowspan="3">AWAMU YA 2<br><br>HUDUMA</td><td colspan="2">Wahudumu wote wanapaswa kuingiza mahudhurio ya EVV kuanzia tarehe 5 Agosti 2019</td></tr>
<tr><td colspan="2">Mpango wa EVV kwa walipaji wafuatao:<br><br>Mashirika ya Utunzaji Unaodhibitiwa yanayolipisha Medicaid (Aetna, United Healthcare, Molina, Centene, Paramount, na CareSource). Utekelezaji wa EVV katika Utunzaji Unaodhibitiwa utafanywa kwa huduma zifuatazo:<br><br>▪ Msaidizi wa Afya wa Nyumbani wa Mpango wa Jimbo<br>▪ Uuguzi wa Afya wa Nyumbani wa Mpango wa Jimbo<br>▪ Tathmini ya RN ya Mpango wa Jimbo<br>▪ UUguzi wa Ondoleo wa HCBS 1915c<br>▪ Msaidizi wa Huduma ya Kibinafsi wa Ondoleo la HCBS 1915c<br>▪ Mhudumu wa Huduma ya Nyumbani wa Ondoleo la HCBS 1915c<br>▪ Uuguzi wa Zamu ya Faragha (PDN)</td></tr>
<tr><td>Idara ya Wazee ya Ohio (ODA):<br><br>▪ PASSPORT - Uuguzi wa Mhudumu wa Huduma ya Nyumbani<br>▪ PASSPORT - Huduma ya Kibinafsi ya Mhudumu wa Huduma ya Nyumbani<br>▪ PASSPORT - Utunzaji wa Kibinafsi<br>▪ PASSPORT - LPN wa Uuguzi wa Ondoleo<br>▪ PASSPORT - RN wa Uuguzi wa Ondoleo<br><br>**Huduma za kujielekezea wenyewe hazijumuishwi katika Awamu ya 2</td><td>Idara ya Ohio ya Ulemavu wa Ukuaji (DODD):<br><br>• Uuguzi wa Ondoleo wa Chaguo za Binafsi (IO)<br>• IO/Mhudumu wa Nyumbani/Utunzaji wa Kibinafsi (HPC)<br><u>Minghairi:</u><br><br>• Hazitatumika kwa huduma za kujielekezea wenyewe<br>• Hazitatumika kwenye sehemu ya kituoni/kwenye samu ya HPC, haitatumika kwa huduma zinazotozwa kwa kutumia kiasi cha kulipa cha kila siku (DBU)</td></tr>
</table>

| Ili kupata toleo la tafsiri ya barua hii, tafadhali tembelea: | |
|---|---|
| Para la versión traducida de esta carta, visite: | 如需本函件的翻译版本，请访问: |
| للحصول على نسخة مترجمة من هذه الرسالة، يرجى زيارة: | Wixii nooca fasiran ee warqadaan, fadlan booqo: |
| С переводом этого письма можно ознакомиться по ссылке: | Pour une version traduite de cette lettre, veuillez cliquer sur : |
| For a translated version of this letter, please visit the link below: | Để xem bản dịch thư này, vui lòng truy cập: |
| Prevedenu verziju ovog pisma potražite na adresi: | Ko larni ɗerewol ndu je lornama, useni ngile: |
| यो पत्रको अनुवाद गरिएको संस्करण निम्ति, कृपया निम्न साइट हेर्नुहोस्: | इस पत्र के अनुवादित संस्करण के लिए, कृपया यहाँ विज़िट करें: |
| https://www.medicaid.ohio.gov/INITIATIVES/Electronic-Visit-Verification | |